/

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA
***(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)***

Kumb. Na. JA.312/322/03/74 26/09/2025

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba

S.L.P 03

**TANDAHIMBA.**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUJITOLEA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anapenda kuwatangazia watanzia wote wenye sifa ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kuomba maombi ya nafasi za kazi ifuatavyo:

**FIZIOTHERAPIA/MTOA TIBA KWA VITENDO DARAJA LA II- NAFASI 1**

**KAZI/MAJUKUMU YA FIZIOTHERAPIA/MTOA TIBA KWA VITENDO**

i. Kutoa tiba kwa kuzoeza viungo kwa vitendo

ii. Kukusanya na kutunza takwimu na taarifa za mgonjwa

iii. Kumchunguza mgonjwa ili kutambua na kupanga tiba kwa vitendo

iv. Kutekeleza tiba kwa vitendo kwa mgonjwa

v. Kutunza vifaa vya Idara

vi. Kutoa elimu ya Afya kwa jamii kuhusu kutambua dalili na kuzuia ulemavu

vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa Wahitimu wa Kidato cha Nne (Form Four) au kidato cha Sita (Form Six) wenye Stashahada (Diploma) ya Fiziotherapia/Mtoa tiba kwa vitendo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**MSHAHARA**
Utazingatia Muongozo wa kujitolea kwa watumishi wa Kada za Afya

**MSHAHARA YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) Watatu wa kuaminika.

iii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuhitimu Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

**iv.** "Testimonial", "Provision Result, "statement of result", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

V. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

**VI.** Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **10/10/2025.**

VII. Maombi yote yaelekezwe kwenye anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba,**

**S.L.P 03,**

**TANDAHIMBA-**

Imetolewa na:

David Sinyanya
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
**TANDAHIMBA**

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S. L. P. 03
TANDAHIMBA